



## TANGAZO KWA UMMA

Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imekamilisha kazi ya kupitia maombi ya kuvuna miti katika mashamba ya kupanda yanayomilikiwa na serikali kuu chini ya usimamizi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS). Uhakiki huo umefanyika katika mashamba nane yenye miti iliyokomaa kuvunwa ambayo ni Sao Hill (Mufindi), Buhindi (Sengerema), Meru/Usa (Arumeru), West Kilimanjaro (Hai), Shume (Lushoto), North Kilimanjaro (Rombo), Kiwira (Rungwe) na Kawetire (Mbeya Vijijini). Mapitio ya kuhakiki maombi yaliyofanyika yamezingatia pamoja na mambo mengine upatikanaji mdogo wa malighafi ya miti ya kuvuna katika mashamba tajwa ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya waombaji. Hivyo, umma unajulishwa kuwa baada ya tathmini ya maombi kufanyika serikali imetoa idhini kutolewa mgao wa kuvuna malighafi katika mashamba ya kupanda kwa mwaka 2016/2017 kwa waombaji kulingana na upatikanaji wa malighafi iliyopo.

Ikumbukwe kuwa tarehe 8 Julai, 2016 Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa ufafanuzi na agizo la kusitisha kugawa miti ya kuvuna katika mashamba yote ya serikali kuu kwa ajili ya kutathmini taratibu, kanuni na vigezo sahihi vinavyotakiwa kutumika katika kugawa malighafi kutoka kwenye mashamba hayo. Pia, aliwataka na kuwashauri wadau wote wa viwanda vinavyojikita katika malighafi ya misitu hususan wamiliki wa viwanda vya kupasua mbao kuwa watulivu wakati utaratibu huu ukifanyiwa mapitio na umma utatangaziwa rasmi pindi uboreshaji huo utakapokamilika.

Kwa sasa serikali inaandaa mazingira bora zaidi ya majadiliano na wamiliki wa sekta ya viwanda vya misitu nchini ili kupata mfumo bora zaidi wa kugawa malighafi ya miti katika mashamba yaliyopo. Aidha, nia ya serikali ni kuweka mfumo madhubuti siku za baadaye kwa ajili ya kuboresha ukusanyaji wa mapato ya

serikali yanayotokana na mazao ya misitu katika misitu yote nchini na kuondoa malalamiko ya ugawaji wa malighafi ya kuvuna.

IMETOLEWA NA:  
KATIBU MKUU  
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII  
S. L. P. 9372,  
MPINGO HOUSE  
DAR ES SALAAM  
JUMATANO, AGOSTI 3, 2016.